TAREKHE YA WANAVYUONI WA ZANZIBAR

SHEIKH ABDALLAH BIN MUHAMMAD BAKATHIR

(1276 – 1343 AH/1860 – 1925 AD)

Jengo la Ukutani alilolliwacha Sheikh Abdallah Bakathir likionekana nyuma ya Mashekhe waliosimama waliokuwa zama za baada yake

SHEIKH ABDALLAH BIN MUHAMMAD BAKATHIR (BUY)

Jina lake

Sheikh Abdallah bin Muhammad bin Salim bin Ahmad bin Ali bin Abdallah bin Omar bin Kadhi Abdur-Rahim Bakathir Al-Kindy. Ameitwa "*Buy*" kutokana na kumwita baba yake hivyo alipokuwa mdogo na likamselelea yeye baadae.

Wazee wake

Babu yake Bwana Salim bin Ahmad ndie aliyehamia Afrika ya Mashariki na akaja akazaliwa baba yake Sheikh Abdallah huko kisiwa cha Lamu. Ama babu yake Kadhi Abdur-Rahim alikuwa ni Kadhi wa Tarim mji maarufu Hadhramout kwa Wanavyuoni tokea kale. Watu wa ukoo huu wa Al-Kindy wapo zaidi maeneo ya Hadhramout na Oman. Mama yake ni Bibi wa Kibaruwany bint Abdallah bin Adiy bin Abdallah.

Kuzaliwa na kulelewa kwake

Sheikh Abdallah amezaliwa mwaka 1276 AH sawa na 1860AD kwenye kisiwa cha Lamu katika mtaa wa Mkomani moja ya mitaa mashuhuri ya Lamu.

Baba yake alifariki wakati yeye akiwa na umri wa miaka sita tu, hivyo aliinukia katika maisha ya uyatima jambo liliomfanya ahangaikie maisha yake akiwa angali ana umri mdogo. Alijifundisha ushoni wa charahani akawa anashona kofia na kanzu na hii ilikuwa ndio kazi yake mpaka utuuzimani kwake ingawa mwisho wake hakuwa akishona yeye bali watu wa nyumbani kwake ndio ikawa kazi yao.

Kusoma kwake

Alisoma kwa Mashekhe wengi sana, wapo wa Lamu kisha wa Unguja, Makka, Hadhramouti na kwengineko.

Mashekhe zake wa Lamu

Lamu katika zama hizo walijaa Wanavyuoni na Wacha-Mungu, hivyo alibahatika kusoma tokea utotoni mwake kwa Mabwana hao walio mashuhuri sana, kati ya hao ni:

1. Sayyid Abubakar Abdur-Rahman Al-Husayny maarufu (Mansab).
2. Sayyid Ali bin Abdallah bin Hasan Jamalil Leyl.
3. Habib Saleh bin Alwy bin Abdallah Jamalil Leyl.
4. Sheikh Muhammad bin Ali bin Mselem Al-Amiry (Kadhi wa Lamu).
5. Sheikh Abubakar bin Muhammad Al-Maawy.

Alisoma kwa Mashekhe hao na wengineo fani kemkem hadi kufikia umahiri mzuri katika fani tofauti zikiwemo za *Fiqhi, Nahau, Hadithi, Tafsiri ya Quran* n.k.

Mashekhe zake wa Unguja

Baadae aliazimia kuelekea Unguja na kupewa maagizo na Shekhe wake Habib Saleh Jamalil Leyl awakusudie Mashekhe kadha na khasa Habib Ahmad bin Abubakar bin Sumeyt.

Alipofika Unguja akasoma kwa Mashekhe hao na khasa kwa Habib Ahmad ambapo alijifunza chungu ya vitabu. Baadhi ya vitabu alivyovisoma kwa Habib Ahmad bin Sumeit tu pekee ni *"Tafsiri ya Jalaleyn", "Qutul- Quluubi" cha Tasawwuf, "Fat-hul*

Jawaad" cha Fiq-hi, na akasoma vitabu alivyotunga Habib Ahmad bin Sumeit mwenyewe.

Miongoni mwa Mashekhe zake wa Unguja ni:

1. Habib Ahmad bin Abubakar bin Sumeyt (Kadhi wa Unguja).
2. Sheikh Abdallah bin Wazir wa Msujini.
3. Sheikh Muhammad bin Ahmad bin Hasan Al-Murony.
4. Sayyid Hassan bin Muhammad bin Hasan Jamalil Leyl.

Mashekhe zake wa Makka

Sheikh Abdallah aliazimia kwenda Makka kufunga kambi kuchota elimu kwa Mabwana wa huko. Shekhe wake Habib Saleh wa Lamu akampa barua ya kumtambulisha kwa Habib Ahmad bin Sumeit Kadhi wa Unguja ili nae amtambulishe kwa Mashekhe wakubwa wa Makka. Nae Habib Ahmad akamjulisha kwa Mashekhe wa huko na kumtaka ashikamane zaidi na Sheikh Omar bin Abubakar Bajuneyd nae Sheikh Abdallah akafanya hivyo alipofika Makka. Alipendeza mno kwa Shekhe huyu hadi Sheikh Bajuneyd alipotakiwa amtume mwalimu akasomeshe Jawa (Indonesia) basi alimtuma Sheikh Abdallah aende huko kusomesha, nae akatekeleza amri hiyo.

Alibahatika kusoma kwa Mashekhe wengi hapo Makka na fani nyingi sana.

Miongoni mwa Mashekhe zake wa Makka ni:

1. Sheikh Omar bin Abubakar Bajuneyd.

2. Sayyid Abubakar bin Muhammad Shatta (*mtunzi wa kitabu cha Hashiya ya "Fat-hul Muiin" inayoitwa "Ianatul Talibiin" juzuu nne na kitabu maarufu cha''Durarul-bahiya''*)
3. Sheikh Muhammad Said bin Muhammad Babsyl (Mufti wa Makka).
4. Habib Husein bin Muhammad bin Husein Al-Hibshy (alikuwa Mufti wa Makka zama zake).

Mashekhe zake wa Hadhramout

Sheikh Abdallah baada ya kurudi Unguja alichota elimu tele kwa Mashekhe zake na ikamjia hamu ya kuwazuru Mabwana wa Hadhramout ili atabaruki nao ndipo Shekhe wake Habib Ahmad bin Sumeit akampa chungu ya barua za kumtambulisha kwa Mashekhe wakubwa wa huko.

Katika safari hii alifuatana na sahibu yake Sayyid Abubakar bin Ahmad bin Sheikh Patte, mwanawe Sheikh Abubakar bin Abdallah Bakathir na Sheikh Muawiya bin Hasan Al-Maawy mtoto wa mama yake mdogo.

Safari hii ilikuwa mwezi 21 Mfungo mosi 1314 AH sawa na tarehe 26 March 1897 AD. Alipita kila maeneo ya Mabwana watukufu na kutabaruku kwa kusoma baadhi ya vitabu mbele yao na kupatiwa Ijaza tele.

Miongoni mwa Mashekhe aliosoma vitabu mbele yao:

1. Habib Ali bin Muhammad Al-Hibshy (Seyun).
2. Habib Tahir bin Abdallah bin Sumeit (Shibam).

3. Habib Abdur-Rahman bin Muhammad Al-Mashuhur (wa Tareem na aliyekuwa Mufti wa Hadhramout).
4. Sheikh Muhammad Baridhwan (Inaat).
5. Sayyid Ahmad bin Muhammad Al-Kaaf (Tareem).
6. Sheikh Ahmad bin Abdallah Al-Khatiib (Tareem).
7. Habib Ubaydillah bin Muhsin Assaqqaf (Seyun) na
8. Habib Ahmad bin Hasan Al-Attas (Hureidha).

Pia amepata Ijaza nyingi kutoka kwa mashekhe tofauti, amewataja katika kitabu cha safari yake hiyo kinachoitwa *"Al-Ashwaqul Qawiyyah ilaa Mawatini Saadatil Alawiyah"*.

Mashekhe zake wa Madina

Sheikh Abdallah Bakathir pia alifika Madina na akabahatika kusoma kwa Sayyid Ali bin Tahir Al-Madany Al-Hanafy.

Kuhamia kwake Unguja

Baada ya kumaliza masomo yake ya Makka alirudi kwao Lamu na huko Mashekhe zake wakamshauri ahamie Unguja na kumwambia kuwa hatopata sehemu nzuri yenye watu wenye tabia njema kama Unguja.

Alipohamia Unguja mwaka 1309 AH sawa na 1892 AD alifikia mtaa wa Hamamni kwa rafiki yake Sheikh Omar bin Muhammad Al-Kahtany na baadae akamuoa binti yake.

Ilipofika mwaka 1320 AH sawa na 1902 AD alinunua nyumba ya Ukutani kwa Sayyid Nassir bin Abdur-Rahman Al-Huseyny. Akawa anasomesha darasa zake ukumbini mpaka baada ya

miaka saba akajenga seble ya kusomeshea watu, ujenzi huo ulifanyika katika mwaka 1909.

Kusomesha kwake Zanzibar

Sheikh Abdallah alisomesha sana Unguja na alikuwa na wanafunzi wengi kupita kiasi, alisomesha vitabu tofauti na fani zote alizozisoma kwa Mashekhe zake alikuwa akizisomesha.

Alikuwa na darsa za kila wakati, watu walimfata Shambani kwake huko Fuoni kwenda kusoma, alisomesha Msikiti Gofu baada ya Magharibi hadi alipofunguwa Madrasa yake ya Ukutani akawa anasomesha Ukutani saa moja asubuhi na Msikiti Gofu akawa anadarasisha mwezi wa Ramadhani tu katika nyakati za Laasiri, zile darasa zake za Magharibi za Msikiti Gofu alimwachia mwanafunzi wake Sheikh Muhammad bin Abdallah Al-Henzuwany. Pia alikuwa na darasa za nyakati tofauti kwa wanafunzi mbalimbali mfano wa darasa ya adhuhuri ya Tafsiri ya Quran ya wanafunzi wake maalumu.

Sheikh Abdallah Bakathir alisomesha watu wengi wa mjini pamoja na mashamba.

Miongoni mwa wanafunzi wake wakubwa ni:

1. Habib Omar bin Ahmad bin Sumeit.
2. Sheikh Abubakar bin Abdallah Bakathir.
3. Sheikh Muhsin bin Ali Al-Barwany.
4. Sheikh Ahmad bin Muhammad Mlomry.
5. Sheikh Muhammad bin Khalfan Al-Filany.
6. Sheikh Muhammad bin Omar Al-Khatiib.

7. Sheikh Muhammad bin Abdur-Rahman Al-Makhzumy.
8. Sheikh Muhammad bin Abdallah Al-Hinzuwany.
9. Sheikh Salim bin Said bin Seif Ash-Shiheby.
10. Sheikh Jabir bin Saleh bin Kassim Al-Farsy.
11. Sayyid Abdallah bin Muhammad Ash-Shatry.
12. Sayyid Habib bin Muhammad Ash-Shatry.
13. Sheikh Said bin Abdallah Lindy.
14. Sheikh Suleyman bin Muhammad Al-Alawy.

Wanafuzni wake wakubwa wa Kenya (Lamu na Mombasa)

Sheikh Abdallah alisomesha pia Lamu na Mombasa wanafunzi wengi, miongoni mwao:

1. Sheikh Abdallah bin Khatib bin Muhammad Al-Khatib.
2. Sheikh Suleyman bin Ali bin Khamis Al-Mazrui.
3. Sheikh Al-Amin bin Ali bin Abdallah Al-Mazrui.

Kusomesha kwake Jawa

Wakati Sheikh Abdallah anasoma Makka kwa Sheikh Omar Bajuneyd alitakiwa na Shekhe wake aende Jawa (Indonesia) kusomesha watu ambao walimuomba Sheikh huyo mtu wa kuwasomesha mambo ya dini yao.

Sheikh Abdallah bila ya kurudi nyuma alikwenda Jawa na akasomesha kwa kipindi kirefu na hakurudi Makka hadi alipoweza kuwasomesha watu ambao wataweza kuwasaidia wenzao. Hivyo Sheikh Abdallah Bakathir amesomesha Jawa na amekuwa na wanafunzi isipokuwa hawakudhibitiwa na kuorodheshwa majina yao.

Vitabu alivyotunga

Sheikh Abdallah hakuwa na vitabu vingi alivyoviandika, muda wake mwingi alikuwa akiutumia kudarasisha. Kati ya vitabu alivyotunga ni:

1. Safari yake ya Hadhramout, Misri, Makka na Madina ambayo ameandika matukio mengi na sehemu nyingi pamoja na kuwataja Mabwana aliowadiriki, safari hiyo ilikuwa mwaka 1314-1316 AH (1897-1898) na kitabu hicho kimeitwa *"Al-Ashwaqul Qawiyyah ila Mawatini Saadatil Alawiya"* na zaidi amewaelezea wale aliokutana nao Hadhramout kuliko maeneo mengine aliyoyazuru.
2. Kitabu kidogo cha kutaja utukufu wa Mtume Muhammad (S.A.W) ambacho mwanawe Sheikh Abubakar akakiita jina *"Kashful-Ghitaa fii Huquuqil Mustafa*".

Safari zake

Sheikh Abdallah alikuwa mwenye kupenda kusafiri sana wakati wa ujana wake na utuuzimani mwake.

Alikwenda Makka kuhiji kisha akaenda tena kwa ajili ya kusoma, pia alifika Madina, Hadhramout, Misri, Jawa (alipopelekwa kusomesha), Uganda, visiwa vya Ngazija, Barawa na Afrika ya Kusini katika mji wa Cape Town ambapo alikwenda huko kwa amri ya Shekhe wake Sheikh Omar Bajuneyd wa Makka baada ya watu wa Cape Town kumuomba Mufti wa Makka Sheikh Muhammad Babsyl awapelekee mtu akasuluhishe mgogoro wa waislamu uliokuwepo huko Cape Town baina ya waumini. Sheikh Abdallah akaenda huko na

akafanikiwa kupatanisha Waislamu wa huko na kuutatua mgogoro wao.

Mafungamano yake na Wanavyuoni

Sheikh Abdallah alikuwa kipenzi cha Mashekhe zake, alipendwa na kuthaminiwa, nae alijuwa kujipendekeza kwao, amekuwa na mawasiliano nao baadhi yao hata pale alipokwisha kusoma kwao na kurudi nyumbani.

Amekuwa na mawasiliano ya kuandikiana barua baina yake na Mashekhe zake kila baada ya muda, mfano wa maandikiano ya barua baina yake na Habib Ali bin Muhammad Al-Hibshy na Sheikh Umar Bajuneyd ambae hakuwacha kumtumia vitu vya kielimu baada ya kurudi Unguja nakadhalika.

Utukufu na baadhi ya sifa zake

Sheikh Abdallah sio tu alipendwa sana na Mashekhe zake bali na watu wengi walikuwa wakimpenda, na wengine wakimtanguliza na kumheshimu kutokana na utukufu aliokuwa nao. Aliishi na Mashekhe zake kama marafiki pamoja na kuwawekea heshima yao ya hali ya juu kabisa khasa Habib Saleh Jamalil Leyl na Habib Ahmad bin Sumeit.

Aliaminiwa kutokana na elimu aliyonayo na umakini wake hadi Habib Ahmad bin Sumeit akamuamrisha mwanawe Habib Omar bin Sumeit aende akasome kwake.

Alikuwa Mcha-Mungu wa kupigiwa mfano, sifa hii ya Ucha-Mungu kwake walikubaliana watu wote watukufu wa zama zake.

Alisifika kwa ukarimu, upole, akipenda wanafunzi wake, alikuwa na Tawadhui, hakuwa akijikweza, alikuwa na himma kubwa ya kusomesha watu na sifa nyenginezo nzuri alizokuwa nazo.

Mambo mazuri aliyoyaacha nyuma yake

Sheikh Abdallah amewacha mambo mengi mazuri, ameichangamsha Unguja kielimu na kusomesha wanafunzi wengi sana. Katika yale mazuri aliyoyawacha nyuma yake ni:

1. Watoto wema na wajukuu wa kheri.
2. Wanafunzi waliokuwa Mashekhe katika kila pembe ya Afrika ya Mashariki.
3. Amekua kiunganishi katika nyanja za elimu ya Dini kwa kuwa alisoma kwa Mashekhe wengi wa Makka, Hadhramout na Afrika Mashariki na kupewa Ijaza kemkem. Hapa ndipo ilikuwa ikielezwa tangu dahari kuwa Elimu ya dini ya Afrika Mashariki ina chimbuko la Wanavyuoni wakubwa wa Ulimwenguni.
4. Ukutani ikiwa ni Madrasa ya aina yake aliyoianzisha akiwasomesha watu wa kila namna, wametoka hapo Wanavyuoni wakubwa aidha alikuwa akisomesha fani zote alizozipata kwa Mashekhe zake, hayo yote yakaifanya Ukutani kuwa ni kituo muhimu kwa Zanzibar katika kuendeleza taaluma ya Dini ya Kiislamu.
5. Darsa za Ramadhani za msikiti Gofu, darsa hizi zimedumu hadi sasa kwa kupokewa na Mashekhe mbalimbali katika kila zama.

6. Sala ya Tarawehe na Witri kwa juzuu katika msikiti Gofu ambayo aliianzisha yeye na kuendelea hadi sasa.

Watoto wake

Sheikh Abdallah alikuwa na watoto wengi lakini waliosimama ni 6 tu, watatu wanawake na watatu wanaume akiwemo Sheikh Abubakar bin Abdallah Bakathir.

Kufariki kwake

Alifariki Unguja usiku wa tarehe 14 Shaaban mwaka 1343 AH sawa na 10 March 1925 AD akiwa na miaka 67.

Alisaliwa msikiti Gofu na Sala iliongozwa na Habib Ahmad bin Sumeit na akazikwa katika kitalu cha Aal Sheikh Abi Bakar bin Salim kilichopo nyuma ya Ukutani.

Zilisomwa Khitma zake kwa muda wa siku tatu katika msikiti wa Ijumaa wa Malindi baada ya Sala ya Isha.

Hakika kifo chake kilikuwa ni msiba mkubwa kwa watu wa Zanzibar na Afrika Mashariki kwa ujumla.

Rejea

1. *Sheikh Abdallah Saleh Farsy "Baadhi ya Wanavyuoni wa Mashariki ya Afrika" cha mwaka 1972.*
2. *"Al-Ashwaqul Qawiyyah" ziara yake ya Hadhramout.*